**Kwa wanafunzi wasichana wa Kiislamu wanaopendelea kuvaa hijabu wanapaswa kuwa na:-**

1. Sketi 2 za rangi ya Maruni (damu ya mzee) ndefu zinazofika katika vifundo vya miguu, zenye marinda tajwa hapo juu.
2. Ushungi 2 nyeupe, pana, ndefu isiyofunika viganja vya mikono, zisifunike uso,visiwe vyepesi na wala visiwe na urembo wowote.
3. Blauzi (Nusu Kanzu) 2 nyeupe za mikono mirefu zisizofunika viganja vya mikono, iwe pana isiyobane, pia iwe ndefu inayoishia juu ya magoti, isiwe kama gauni na isiwe nyepesi.
4. 'Over – Coat' 1 la rangi ya 'Dark Blue'.
5. Soksi nyeupe jozi 2.
6. Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 visivyokuwa na kisigino kirefu wala kuchongoka mbele. Lazima viwe vya kufunga kwa kamba
7. Sweta 1 ya mikono mirefu ya rangi ya Maruni (Damu Ya Mzee) yenye shingo ya V.

**(ii) WAVULANA;**

1. Suruali 2 za rangi ya Maruni (Damu Ya Mzee) **zisiwe za kubana** (vibamba) na ziwe na **marinda mawili**.
2. Mashati 2 meupe ya mikono **mifupi**
3. 'Over-Coat' moja la rangi ya Dark blue.
4. Soksi nyeupe jozi 2
5. Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 visivyokuwa na kisigino kirefu wala kuchongoka mbele. Lazima viwe vya **kufunga kwa Kamba**.
6. Sweta 1 ya mikono mirefu ya rangi ya Maruni (Damu Ya Mzee) yenye shingo ya V.
7. Mkanda mweusi usiwe mpana sana wala usiwe na Bakoli/Chata kubwa ya kubandika.

**B. MAVAZI YA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS) NA MICHEZO;**

(i) WASICHANA;

1. Sketi 2 nyeusi ziwe na marinda 16 (nane kila upande) yaliyopangwa kuelekea kulia na ziwe ndefu za kufunika goti.
2. Tisheti 2 Nyekundu au Kijani na zisiwe na maandishi au chata yoyote.
3. Track suti ya rangi ya Bluu bahari
4. Tisheti zenye nembo ya shule ambazo mwanafunzi ataruhusiwa kuivaa ndani na nje ya shule, Gharama yake ni Tsh. **11,000/=.** (zinapatikana kwenye duka la shule )
5. Kwa wasichana wa kiislamu wanaopenda kuvaa **Hijab,** hijab zinapaswa kuwa za rangi nyeusi zinazoishia kifuani na zisiwe na urembo wowote.

(ii) WAVULANA;

1. Suruali 2 nyeusi zenye marinda mawili, iwe ndefu na isiwe ya kubana (Kibamba)
2. Tisheti 2 nyekundu au kijani na zisiwe na maandishi au chata yoyote.
3. Track suti ya rangi ya Bluu Bahari

